

Kituo cha Kupona Maafa huko Davenport Kufunga Oktoba 16

Release Date: Oktoba 15, 2020

Msaada bado una patikana kwa waathirika wa derecho

DES MOINES, Iowa – Kituo cha Kupona Maafa cha FEMA kitafungwa huko Davenport Ijumaa, Oktoba 16 saa 6 asubuhi. Walakini, msaada kwa manusura wa derecho ya Agosti ni kupiga simu tu, bonyeza kamputa au gonga mbali kwenye programu ya FEMA.

DRC iko katika Kituo cha Majini cha Annie Wittenmyer Family (Annie Wittenmyer Family Aquatic Center) kilicho katika:

2828 Eastern Ave.

Davenport, IA 52803

(Kwenye kona ya Mashariki ya 29th St. na Mashariki Ave.) East 29th St. na Eastern Ave.

Walionusurika hawa lazimiki kutembelea DRC kusajili au kuwasilisha hati kwa FEMA.

Waombaji wanaweza kujiandikisha kwa njia zifuatazo:

- Nenda mkondoni kwa [DisasterAssistance.gov](https://www.disasterassistance.gov).
- Pakua App ya Simu ya FEMA ([FEMA Mobile App](#)) kwenye simu mahiri (smartphones).
- Piga simu 800-621-3362 (TTY: 800-462-7585) kati ya saa 6 asubuhi na 10 jioni. Saa za Kati (Central Time), siku saba kwa wiki. Waendeshaji kazi wa lugha nyingi wana patikana.

Nyaraka pia zinaweza kuwasilishwa kwa njia yoyote ifuatayo:



FEMA

Page 1 of 2

- Tume Barua kwa Mpango wa Watu binafsi na Kaya wa FEMA, Kituo cha Huduma cha Usindikaji cha Kitaifa, National Processing Service Center, P.O. Box 10055, Hyattsville, MD 20782-7055.
- Tuma fks kwa 800-827-8112.
- Wasilisha kupitia akaunti ya mtandao ya FEMA. Kuanzisha akaunti mkondoni, tembelea DisasterAssistance.gov, bonyeza "Angalia Hali" (check status) na ufuate maelekezo.

Utawala wa Biashara Ndogo ya Amerika (SBA) hutoa mikopo ya shirikisho ya riba ya chini kwa wafanya biashara wa ukubwa wote, mashirika mengi ya kibinafsi yasiyo ya faida, wamiliki wa nyumba na wapangaji.

Uomba kwa <https://disasterloanassistance.sba.gov>. Watu wanaweza pia kupiga 800-659-2955 au barua pepe FOCWAssistance@sba.gov. Watu viziwi au wasikiaji ngumu wanaotumia TTY wanaweza kupiga simu 800-877-8339.

Walio nusurika katika Benton, Boone, Cedar, Clinton, Jasper, Linn, Marshall, Polk, Poweshiek, Scott, Story na Tama, kaunti zina hadi Novemba 2 kuji andikisha kwa msaada wa maafa.



FEMA

Page 2 of 2